

■ MWANZA

# Maji ya Ziwa Victoria hatari

Na **BENJAMIN MASESE**

MAJI ya Ziwa Victoria yataendelea kuwa machafu na kina chake kupungua kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu ambazo hufanywa bila kuzingatia sheria za utunzaji mazingira, imeelezwa.

Kauli hiyo ilitolewa Mwanza mwishoni mwa wiki na Mtalaamu wa Mradi wa Uhifadhi Mazingira wa Bonde la Ziwa Victoria (LVEMP II), Anna Masasi.

Alikuwa akiwasilisha taarifa yake katika mkutano ulioandaliwa na Taasisi ya Konrad Adenauer Stiftung (KAS) kwa kushirikisha nchi za Afrika Mashariki.

Masasi alisema kuna tishio kubwa la maji yote ya ziwa kuchafuku na kina kupungua kutokana vyombo vya usafirishaji kumwaga mafuta na kutokuwapo mfumo wa kuhifadhi kinyeshi.

Aliitaka Serikali kufanya ukaguzi

kujua vyombo hivyo vinatupa wapi uchafu wao.

Pia alisema taka ngumu za binadamu wanaoishi katika mabonde na mito inayoingiza maji yake Ziwa Victoria ni miongoni mwa vyanzo vinavyosababisha maji kuchafuka na kina kupungua ambacho ni wastani mita 80.

Masasi alisema sababu nyingine ni viwanda, magugu maji na mialo ambayo kwa kiasi kikubwa inazalisha uchafu na taka za aina nyingi na uko-sefu wa vyoo na maji safi.

“Sote tunajua asilimia 80 ya maji ya Ziwa Victoria yanatokana na mvua, isiponyesha hayaongezeki.

“Idadi ya watu wanaotegemea ziwa inaongezeka kila siku, kibaya zaidi kati ya mialo 642 iliyozunguka ziwa ni mialo 43 tu yenye mfumo wa vyoo na maji safi.

“Sasa angalieni idadi ya mialo iliyobaki inafanya uchafuzi, pia katika viwanda vinavyozingatia mfumo ya uhifadhi mazingira ni 118

lakini tukumbuke kuna makundi mengine ya mifugo na kilimo cha mabondeni,” alisema.

Hata hivyo alisema Tanzania imekuwa ikipata fedha ambazo hufikia kati ya dola milioni 360 hadi 400 kwa mwaka kutokana na shughuli za uvuvi.

Alisema Tanzania inapaswa kuelelea na mikakati yake ya kuzalisha umeme Wilaya ya Ngara unaotokana na ziwa kama ilivyo Uganda.

Baadhi ya wachangiaji wa mada mbalimbali za utunzaji wa mazingira, walipendekeza nchi zote za EAC kuwa na mpango wa kuweka vyoo vinavyotembea katika mialo (mobile toilet) i kupunguza uharibifu ndani ya ziwa.

Mkuu wa Programu wa Mabadi-liko na Usalama wa Nishati Kusini mwa Janga wa Sahara kutoka KAS, Oliver Puppel alizitaka nchi za EAC kuweka mikakati ya kuhifadhi Ziwa Victoria kwa manufaa ya kizazi cha cha sasa na kijacho.